Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 6, Issue 3
17th Safar 1432
21st January, 2011

SWALA YA KUOMBA MVUA (*SWALAAT AL-ISTISQAA'*)

Mtayarishi: Sheikh Abu 'Abdir-Rahmaan 'Aadil Bin Yusuf al-Azzaazy

Nukta Ya Kwanza: Maana ya al-Istisqaa' katika lugha ya kiarabu ni mtu kutaka kunyweshwa maji. Na maana ya kisheria ni kumuomba Allaah atuletee mvua wakati kunapotokea ukame (chaka) kwa njia makhususi.

Nukta Ya Pili: Hukmu inayohusiana na swala hii ni katika sunnah *mu'akkadah* (zilizokokotezwa).

Sampuli Yake Inavyoswaliwa: 'Aaisha (رضي الله عنها) amesimulia yakwamba watu walimlalamikia Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusu ukosefu wa mvua na Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaamrisha aletewe minbar. Akawekewa minbar katika *Muswallaa* na akenda hapo wakati jua lilipochomoza, akapanda juu ya minbar hiyo na kupiga Takbira, akamuhimidi Allaah (*akasema Alhamdulillaah*) kisha akasema: "Kwa hakika nyinyi mnalalamika kuhusu ukame wa sehemu mnazoishi na Allaah amewaamrisha mumuombe na akawaahidi kuwa atawajiibu, kisha akasoma (*Du'aa' hii*): '*Alhamdulillahi rabbill-'Aalamin Arrahmanirrahim Maliki yawmiddin la ilaha-illallaah yaf'alu maa yu-reed Allaahumma antallaah laa-illaaha illaa-anta, antal–ghaniyy wa nahnu-l-fuqaraa' anzil alainal-ghaytha. Waj'al maa-anzalta alaina-Quwwatan wabalaghna illahin.*' Kila jinsi ya Sifa njema inamstahili Allaah, Mola wa viumbe vyote. Mwenye kurehemu wema na wabaya hapa duniani, Mwenye kurehemu wema watupu kesho Aakhera, Mwenye kumiliki siku ya malipo. Hapana anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah. Hapana anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni Wewe. Wewe ni mkwasi (tajiri) na sisi ni mafukara. Tuteremshie mvua na ujaalie utakacho kiteremsha kwetu ni nguvu na akiba itakayotufikisha mwisho wa maisha yetu). Kisha akainua mikono yake na akaendelea hivyo mpaka weupe wa makwapa yake ukaonekana. Kisha akawageuzia watu mgongo wake akakigeuza kishali chake haliyakuwa ameyainua mikono yake. Kisha akawaelekea watu na akateremka na akaswalisha rakaa' mbili. Allaah akaleta wingu (la mvua), likapiga radi na umeme ukamemetuka, kisha mvua ikanyesha." [Amepokea Abuu Dawud na Isnad yake ni jayyid]. Na katika riwaya nyengine ya hadeeth, alipoona haraka zao (yaani za maswahaba) za kwenda nyumbani, alicheka mpaka meno yake yakaonekana; akasema: "*Nashuhudia hakika ya Allaah juu ya kila kitu ni Muweza, na hakika yangu mimi ni mja wa Allaah na Mtume wake.*" [Abu Dawud 1173; akaitia katika kitengo cha hadeeth *hasan* al-Albaani katika *Al-Mishkaat Ibnu Hibbaan* 2860 na wengineo].

Na vile vile amesimulia 'Abdullaah Bin 'Abbaas (رضي الله عنهما) alipoulizwa juu ya *Swalaat al-Istisqaa'*: "Alitoka Mtume (صلى الله عليه وسلم) (kwenda kuswali *al-Istisqaa'*) akiwa amevaa nguo zilizotakalika haliyakuwa na sauti ya unyenyekevu. Akawa anatembea kwa utaratibu mpaka alipofika *muswalla* (mahali panaposwaliwa swala hiyo ya *al-Istisqaa'* na Idd) akawekewa mimbar. Hakukhutubu kama khutba yenu hii lakini hakuasa kuleta *du'aa'* na kumnyenyekea Allaah na kuleta takbir kwa wingi (aliendelea kusema hivyo kwa muda) kisha akawaswalisha rakaa' mbili kama anavyowaswalisha 'Idd." Na kwa yale yaliyotangulia yaliyotokamana na hadeeth za Mtume (صلى الله عليه وسلم), yawezekana kuifupisha swala hii kwa namna ifuatavyo: Imaam (kiongozi) atawaahidi watu siku maalum watoke wende katika *muswalla* ili kutekeleza swala hii kwa jamaa'ah na ni Sunnah iwe ni wakati jua linapochomoza; mfano wa swala

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

Yaliyomo

SWALAAT AL-ISTISQAA' 1– 4

SWALA YA KUOMBA MVUA (*SWALAAT AL-ISTISQAA'*)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

ya 'Idd. Namna ya kutoka kwao kwenda *muswalla* awe killa mmoja wao ametoka haliyakuwa amevaa nguo zilizochakaa (kuukuu) kuonyesha udhalilifu wao kwa Allaah. Haliyakuwa ni mwenye kudhihirisha unyenyekevu na utwevu wakati watakapokuwa wanamuomba Allaah haja zao. Imaam atapanda Minbar amuhimidi (amtukuze) Allaah na kukithirisha *du'aa'* na kudhihirisha unyenyekevu wao kwa Mola wao. Wakiwacha kuvaa nguo za fakhri na nzuri kwa kumnyenyekea (Allaah). Kisha atainua (khatibu) mikono yake na ataugeuza mgongo wake kwa watu (aelekee kibla) na akibadilishe kishali chake. Kisha ataswalisha rakaa' mbili kama anavyoswalisha swala ya 'Idd. Na dhahir ilivyo ni kwamba ataleta takbeer (saba katika rakaa ya kwanza na tano ya pili) na hii ndiyo Qauli ya Madh-hab ya *ki-Shaafi'ee,* lakini jamuhuri ya wanavyuoni wamesema yakwamba hakuna takbir. Na qauli ambayo ni *raajih* (yenye nguvu) ni hiyo ya madh hab ya *ki-Shaafi'ee*.

UZINDUSHI: Wamekhitilafiana wanazuoni juu ya itakayoanza mwanzo; [ni Khutba au ni Swala]? Qauli waliyokwenda nayo jamhuri ya wanavyuoni ni kuwa Imaam ataanza kuswali kama swala ya 'Idd mbili na imethubutu uwazi wa jambo hilo (la kuanza kuswali) katika hadeeth ya 'Abdullaah bin Zeid. Na Qauli ambayo ni *Raajih* (yenye nguvu) ni kwamba yafaa kutanguliza au kuakhirisha (ima ukaanza na khutba kisha swala au ukaanze na swala kisha khutba). Hakika imethubutu kutoka katika hadeeth ya Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) na bibi 'Aaisha (رضي الله عنها) yakwamba: "Hakika yeye Mtume (صلى الله عليه وسلم) alianza na khutba na katika hadeeth aloipokea swahaba Abdullaah Bin Zayd (رضي الله عنه) ni kwamba aliswali kisha akakhutubu."

Sifa (namna ya) Kuinuwa Mikoni Katika Du'aa'

Imepokewa kutoka kwa swahaba Anas bin Maalik (رضي الله عنه): "Hakika yake yeye Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliinua mikono yake mpaka nikaona weupe wa makwapa yake." [al-Bukhari 1030 na Muslim 894] na katika Muslim: "Hakika ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliomba mvua, akaashiria kwa kuvielekeza mbinguni vitengele vyake vya mikono)." Na katika riwaya ya Abee Dawud, alikuwa akiomba mvua namna hii: Akanyoosha mikono yake, akaelekeza matumbo ya vitengele vyake vya mikono kwenye ardhi mpaka nikaona weupe wa makwapa yake. Haya yote yaonyesha yakuwa nama gani alivyoinuwa mikono yake kupita kiasi mpaka ikawa matumbo ya vitengele vikielekea ardhini na sehemu yake ya nje akielekeza mbinguni mpaka akawa ni mwenye kuonekanwa weupe wa makwapa yake haliyakuwa ameelekea kibla.

NAMNA YA KUKIGEUZA KISHALI (Kashida): Nako ni kule kugeuza upande wa kulia ukakigeuza upande wa kushoto na kushoto upande wa kulia.

Wasema wanazuoni: "Na hikma ya kufanya hivyo ni kutaraji kwa Allaah kuzibadisha hali. Amma wakati wa kugeuza kishali inakuwa ni pale khatibu anapoelekea kibla kama ilivyopokewa kutoka kwa Abdullah bin Zayd Al Maazini asema: 'Alikuja Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika *Muswalla* akaomba mvua na akageuza kishali chake wakati alipokuwa akielekea kibla.'" [al-Bukhari 1012, Muslim 894 na Abu Dawud 1167]. Na ni Sunnah kwa Imaam kusoma kwa sauti katika swala kulingana na hadeeth iliyothubutu kutoka kwa Swahaba 'Ubbaad bin Tameem kutoka kwa 'Ammi yake (رضي الله عنه): "Hakika ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliomba mvua kisha akaswali rakaa' mbili na kudhihirisha kisomo chake (yaani alisoma kwa sauti)."

Atasoma Nini Katika Swala?

Haikupokewa katika hili la kuswali swala ya mvua hadeeth swaheeh ya kisomo fulani au kusoma sura fulani, lakini yafahamika kutokana na kauli yake Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa alikuwa akiswali 'Idd, husoma (Imam) katika rakaa' mbili hizo zile sura asomazo katika swalaatul 'Idd na vile vile yafahamika kuwa ataleta zile takbira (katika swala) kama anavyoleta katika swala ya 'Idd.

SWALAATUL ISTISQAA' HAINA ADHANA WALA IQAAMA: Kinyume na swala ya *Kusoof* (ya kupatwa jua au mwezi), hii ndiyo peke yake hunadiwa kwa *Asswalaatul Jaami'ah*.

JEE IMAAM ATAPANDA MINBAR (Wakati Wa Kutoa Khutba)?

Dhwaahir yaonyesha yafaa na kujuzu

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

SWALA YA KUOMBA MVUA (*SWALAAT AL-ISTISQAA'*)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

hilo kutokana na hadeeth ilotangulia ya bibi 'Aaisha (رضي الله عنهما) na Ibnu Abbaas (رضي الله عنهما).

DU'AA' ZA KUOMBA MVUA:

Zimepokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) *du'aa'* za kuomba mvua. Miongoni mwazo ni: '*Allaahumma Sqinaa Ghaythan Mughythan Naryan Mury'an Twabqan Ghadqan Aajilah Ghayra Raa ith*.' Maana yake [Ewe Mola tunyesheleze mvua yenye kututoa sisi katika shida, yenye mwisho mzuri (isoleta maangamivu), yenye mazao. Yenye kuenea kwenye miji kwa kheri iliyo nyingi, isonyesha kwa utaratibu (yaani mvua inyeshayo kwa wingi wala sio kidogo kodogo). Na miongoni mwa *du'aa' za* mvua ni ile iliyotajwa mwanzoni mwa makala haya, hadeeth ya bibi 'Aaisha (رضي الله عنهما). Na miongoni mwa dua za mvua ni hadeeth aliyoipokea akisema: "*Allaahumma Sqi Ibaadaka Wa Bahaaimaka Wanshur Rahmataka Wa Ahyi Baldakal Mayyit*." Yaani [Ewe Mola! wanyeshee mvua yako waja wako na wanyama wako. Na uzieneze Rehma zako na uhuishe mji wako ambao utakufa (kwa kukosa mvua]. Na miongoni mwa dua za mvua amepokea Imaam al-Bukhari 1032, Ibnu Maajah 3890: "*Allaahumma Aghythna Allaahumma Aghythna*." Ewe Mola tunyeshee mvua, tunyeshee mvua.

DU'AA' ANAYOISOMA MTU AKIIONA MVUA (inaanza kunyesha): Amepokea bibi 'Aaisha (رضي الله عنهما) yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) anapoona mvua husema: "*Allaahumma swayyiban naafi'an*." [Bukhari 1032; Ibnu Maajah 3890; an-Nasaa'ee 3/164]. Ewe Mola ijaalie yenye kumiminika yenye kunufaisha.

Imepokewa kutoka kwa Anas bin Maalik (رضي الله عنه) yakwamba amesema: "Iilitupata sisi mvua (yaani ilitunyeshea) haliyakuwa tukiwa pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم). Akaifungua nguo yake mpaka ikapatwa na mvua, tukasema kumwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم); 'Kwanini umefanya hivi'? Akasema: "*Ni kwa sababu inaanza kutoka kwa Allaah (sasa hivi hali ya kuwa safi)*.'" [Muslim898, Abu Dawud 5100; Ahmad Ibn Hibbaan]. Na wakati itakapokuwa nyingi ikaleta mafuriko mpaka kukhofia kuleta maangamivu, alikuwa akiomba kwa *du'aa'* ifuatayo: "Allaahumma hawaa 'alayna walaa 'alayna. Allaahumma alal aakaam, wadhwaraab wa butuu nil audiya wa manaabiti shajar. [al-Bukhari 1013, Muslim 898, Abu Daud 1174 - 1175]. Ewe Mola inyesheze kwetu wala isiwe yenye kutuangamiza, Ewe Mola inyesheze kwenye vichaka na Milima na mabonde na kwenye mizizi ya miti.

NJIA NYENGINE ZA KUOMBA MVUA

Zimekuja njia nyengine za kuomba mvua kinyume na zilizotangulia, miongoni mwazo ni: Kuingia khutba ya al-Istisqaa' na swala yake ndani ya swala ya ljumaa itakapoafikiana kutokea katika siku ya ljumaa. Amepokea Anas (رضي الله عنه): "Mtu mmoja aliingia msikitini siku ya ljumaa kupitia mlango wa upande wa daarul qadhaa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa amesimama akihutubu. Akaumuelekea Mtume (صلى الله عليه وسلم) hali ya kuwa amesimama, kisha akasema (yule mtu)! "Ewe Mtume wa Allaah, mali zimeangamia ndia zimekatika, muombe Allaah atupe mvua." Asema, "Akainua Mtume mikono yake kisha akasema. 'Ewe Mola, tunyeshee, Ewe Mola tunyeshee mvua." Asema Anas, "Wallaahi hatukuwa tuneona katika mbingu mawingu ya mvua wala vipande vya mawingu ya mvua na wala hakukuwa kati yetu sisi na jabali la salii nyumba au majengo ya watu (tulikuwa twaliona jabali moja kwa moja)." Akaendelea Anas, "likatokeza nyuma ya jabali, wingu mfano wa duara, lilipotandazika mawinguni likaenea kisha mvua ikaanza kunyesha." akasema: "Wallaahi hatukuliona jua wiki nzima (mvua ilinyesha bila ya kusimama tokea siku ile ya ljimaa). Kisha akaingia mtu siku ya ijumaa iliyofuata kwa mlango ule ule alioingilia nao ljumaa ya kwanza haliyakuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa amesimama yuahutubu. Akamkabili Mtume haliyakuwa amesimama, akasema, "Ewe Mtume wa Allaah, mali zimeangamia, ndia zimekatika, muombe Allaah aizuie." Akainua Mtume (صلى الله عليه وسلم) mikono yake kisha akasema kwa kuomba dua hii: "*Allaahumma hawaa 'alyna walaa 'alayna Allaahumma alal aakaam wadhwaraab wa butuunul audiya wa manabiti shajara*." Ewe Mola inyesheze kwetu wala isiwe yenye kutuangamiza, Ewe Mola inyesheze kwenye vichaka

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

na milima na mabonde na kwenye mizizi ya miti. Ikakatika mvua (ikapusa) tukatoka haliyakuwa ni wenye kutembea kwa miguu. Kwa njia hii, itatosha kuleta *du'aa'* ya kuomba mvua katika khutba ya ljumaa na kuinua mikono yake khatibu na kuinua mikono yao watu wakati wa kuitikia *du'aa'* pamoja na Imaam. limepokewa hili katika moja ya riwaya za al-Bukhari. Fahamu yakwamba wakati mwengine usokuwa wa kuomba mvua, haifai kwa khatibu akiwa juu ya minbar, wala ma'mum kuinua mikono yao wakati wa *du'aa'* na waaitikie "*Aameen*" katika nyoyo zao bila ya kuinua sauti zao. Na vile-vile katika hali hii ya kuomba mvua katika khutba, Imaam hatogeuza kishali chake wala hatolekea kibla wakati wa *du'aa'*. Hili atalifanya wakati atakapo kuwa yuaswali swalatul Istisqaa' yenyewe, ama akiwa katika khutba hatofanya haya. Na miongoni mwa sampuli za kuomba mvua ni kuomba Imaam dua ya mvua isokuwa siku ya ljumaa na bila ya kuswali swala yoyote, sawa ndani ya msikiti au nje kama ilivyokuwa katika hadeeth aloipokea Imaam Abu Dawud 1169 kutoka kwa Swahaba Jaabir Bin 'Abdillaah (رضي الله عنه) asema: "Alimjilia Mtume bwana mmoja akimlalamikia kuhusu ukame. Akaomba Mtume (صلى الله عليه وسلم): *Allaahuma sqinaa ghaythan maryan naafian ghayrydhwaar aajilah ghayru aajil dhwaar aajilan ghayru aajil .*"

VIZUNDUSHO

Kwanza: Jua, Allaah akurehemu yakwamba miongoni mwa sababu za kuzuiliwa mvua ni kumu'asi kwao wanadamu Mola wao kwa kupunja katika vipimo na mizani na kuzuia kutoa zaka za mali zao. Amepokea Ibn Umar (رضي الله عنهما) yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Enyi kongamano la muhaajirin, mambo matano mutakapo onjwa nayo na najilinda kwa Allaah yasije yakawafuata:*

* *Hautokuwa ni wenye kudhihiri uchafu miongoni mwa watu mpaka wakautangaza uchafu huo, isipokuwa utaenea kwao ugonjwa mbaya ambao haukuwepo kwa wale walokuwa kabla yao.*
* *Hawatakuwa watu ni wenye kupunguza vipimo vyao vya mizani wakati wanapofanya biashara isipokuwa wataletewa baa la njaa na kudhalilishwa na kugandamizwa na viongozi wao.*
* *Hawatakuwa ni wenye kuzuia kutoa zaka zao isipokuwa watazuiliwa mvua kutoka mbinguni na lau kama si wanyama hamungenyeshewa mvua.*
* *Hawatokuwa ni wenye kuvunja ahadi za Allaah na Mtume wake isipokuwa Allaah atawaadhibu kupitia kwa maadui zao na kuchukia vile ambavyo walivyo navyo (wanavyovimiliki).*
* *Hawatohukumu viongozi wao na hukumu nyengine isokuwa ya Allaah illa ataweka utesi baina yao (wasisikizane, wapigane wenyewe kwa wenyewe).*

Pili: Jua, Allaah akurehemu! Ni Sunnah kuwatanguliza watu wema wachaji Mungu katika *Du'aa'*. Amepokea Anas (رضي الله عنه): "Hakika 'Umar Bin al-Khataab alikuwa kunapotokea chaka (ukame) akimtaka 'Abbaas bin 'AbdulMutwalib awaombee *du'aa'* akasema, 'Ewe Mola, hakika sisi tulikuwa tukiomba *du'aa'* kupitia kumwambia Mtume wako (صلى الله عليه وسلم) na ukitupa mvua. Na hakika sisi (hivi sasa baada ya kufa yeye) twaomba kupitia kwa 'ammi wa Mtume wako, basi tupe mvua na Allaah akiwateremshia mvua. Wala si makusudio ya *Tawassul* hii kwa Allaah kuwa kutuwassal (kuomba) kupitia kwa dhati ya mtu au jaha yake kama ilivyo kwa watu wengi wasoifahamu hadeeth hii. Na kauli yenye nguvu ni kwamba *tawassul* ilokusudiwa na kutaka kuombewa *du'aa'* kutoka kwake na wala hawakutawassal kwa dhati yake wala jaha yake. Na dalili ya hili limepokewa kwa ndia tofauti:

* Imaam al-Bukhari (رضي الله عنه) amepokea hadeeth katika swaheeh yake chini ya mlangi wa "Watu kumuomba Imaam wamuombe Allaah mvua panapoingia chaka (ukame).
* Neno la 'Umar (رضي الله عنه): "Sisi tulikuwa tuki-*tawassal* (tukaomba) kwako Wewe kupitia kwa Mtume wako)." Yafahamika katika kule kuomba kupitia kwa Mtume. (kwa kumwambia "tuombee") mvua na hadeeth zilizokuja katika Bukhaari na Muslim na Sunna zaonyesha yakuwa walimtaka Mtume (صلى الله عليه وسلم) awaombee *du'aa'* na wala hawaku-*tawassal* kwa dhati yake wala jaha yake.
* Lau kama ku-*tawassal* (kuomba) kwa dhati na jaha yajuzu hawangewacha ku-*tawassal* na Mtume na kwenda kwa Abbas wangetawassal moja kwa moja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم).